# Kifaa Maalum cha Kutazamia Jua:

## Maelekezo ya kutumia






*Kupatwa kamili kwa jua*

*Jumatatu, 21 Agosti 2017*

© 2014-2017
Eclipse2017.org, inc.

# TERMS AND CONDITIONS FOR USE OF SOLAR VIEWER

**Please read these Instructions for Use carefully before using the Solar Viewer. Your purchase and use of the Solar Viewer constitutes your agreement to these terms and conditions. Failure to follow these Instructions for Use may result in serious personal injury, including permanent eye damage. If you do not understand these Instructions or cannot follow them diligently and completely, then you should not look at the Sun at any time, with or without a Solar Viewer.**

The term "Solar Viewer" refers to the special cardboard-and-polymer optical products, marked "SAFE FOR DIRECT SOLAR VIEWING", manufactured by Rainbow Symphony of Reseda CA, and sold by Eclipse2017.org for the purpose of viewing the Sun during the solar eclipse of August 21, 2017, by or under the direct supervision of a person 18 years of age or above and in accordance with these Instructions for Use.

Observing the Sun directly, without the benefit of eye protection provided by the Solar Viewer, will likely result in serious personal injury, up to and including permanent eye damage and blindness. When these Instructions for Use are followed completely and precisely, the undamaged and unmodified Solar Viewer has been proven to be safe and effective in allowing direct, short-term, viewing of the Sun. If these Instructions for Use are not followed, or if damaged or modified Solar Viewers are used, permanent eye injury could result.

You should never look directly at the Sun, with or without the aid of the Solar Viewer, if you have any temporary or permanent medical or other condition which either (1) prevents your use of the Solar Viewer according to these Instructions for Use, or (2) which predisposes you to an increased or special risk of incurring, worsening, or contributing to the effects of any optical or other medical, health, or other condition, by looking or attempting to look at the Sun.

You should never attempt to perform any other activity (such as driving or walking) while using the Solar Viewer.

You agree that if you let others use the Solar Viewer, you will provide each such user with a copy of these Instructions for Use and will make sure such user reads and understands the Instructions for Use before using the Solar Viewer.

By using the Solar Viewer to view the Sun, you agree with the following:

(a) you understand these Instructions for Use completely;
(b) you understand and accept the risks associated with improper use of the Solar Viewer;
(c) you accept full responsibility for, and assume all risks associated with, the act of viewing the Sun, with or without the use of the Solar Viewer; and
(d) the Solar Viewer is fragile and any damage to it or modification of it will render it immediately and permanently unusable for its intended purpose.

Release and Limitation of Liability

By way of purchasing and using the Solar Viewer, you are irrevocably releasing, indemnifying, and holding harmless the manufacturer and seller from any liability, loss, claim and expense (including attorney's fees), including but not limited to bodily injury or other personal harm, which may result from using the Solar Viewer under any circumstances or conditions and irrespective of jurisdiction. Neither the manufacturer nor the seller will be responsible for any damages of any kind, irrespective of reasons, conditions or circumstances, including malfunctioning of the Solar Viewer. All risks associated with using the Solar Viewer rest solely and entirely with the user, irrespective of whether the Solar Viewer is used by the original purchaser or any third party. You fully understand and assume the risks in using the Solar Viewer. You confirm that you have read this release of liability and fully understand its terms and that you have given up substantial rights by purchasing and using the Solar Viewer.

THE MANUFACTURER AND SELLER OF THE SOLAR VIEWER MAKE NO WARRANTY OF ANY KIND, EXPRESSED OR IMPLIED, WITH RESPECT TO THE SOLAR VIEWER, INCLUDING BUT NOT LIMITED TO THE IMPLIED WARRANTIES OF MERCHANTABILITY, FITNESS FOR A PARTICULAR PURPOSE, AND NON-INFRINGMENT. NEITHER THE MANUFACTURER NOR THE SELLER SHALL BE LIABLE FOR ANY OTHER DAMAGES, INCLUDING BUT NOT LIMITED TO DIRECT, INDIRECT, INCIDENTAL, SPECIAL, CONSEQUENTIAL, OR EXEMPLARY DAMAGES, WHETHER IN AN ACTION IN CONTRACT OR TORT (INCLUDING NEGLIGENCE AND STRICT LIABILITY), SUCH AS, BUT NOT LIMITED TO, LOSS OF ANTICIPATED PROFITS OR BENEFITS RESULTING FROM, OR ARISING OUT OF, OR IN CONNECTION WITH THE USE OR FURNISHING OF THE SOLAR VIEWER OR THE PERFORMANCE, USE OR INABILITY TO USE THE SAME, EVEN IF THE MANUFACTURER OR SELLER HAS BEEN ADVISED OF THE POSSIBILITY OF SUCH DAMAGES. IN NO EVENT WILL THE MANUFACTURER'S OR SELLER'S TOTAL LIABILITY EXCEED THE PRICE PAID FOR THE PRODUCT.

Note Regarding Translations

Translations of these Instructions for Use into various languages are provided "AS-IS" and solely for the convenience of the reader. Eclipse2017.org has made reasonable efforts to ensure the accuracy of the Translations; however, in the event of any perceived discrepancy in meaning or interpretation between the English version and any Translation, the English version will prevail. You should not act in reliance on anything contained in any Translation of these Instructions for Use, but should refer to the official English version.


*© 2016-2017*
*Eclipse2017.org, inc.*


# KUPATWA KAMILI KWA JUA - 21 Agosti 2017

**Karibu Marekani!**

Tuna furaha kuwa umetembea nchini mwetu ili kushuhudia tukio kamili la kupatwa kwa jua na tungependa kila mmoja aweze kujionea tukio hili la kuvutia kwa njia iliyo salama!

*Tunatoa ushauri huu kwa Kiswahili kwa manufaa yako. Toleo la ushauri, maagizo na taarifa ya makataa ("Maelezo") haya kwa lugha ya Kingereza ndiyo chanzo cha kina na rasmi cha habari na mwongozo wa matumizi mema na yanayofaa kwa Kifaa Maalum cha Kutazamia Jua ili kuweza kuangalia jua mojakwa moja. Maelezo haya yanapatikana http://tinyurl.com/viewer-instructions na ni sharti uyasome, uyaelewe na uyazingatie ili kutumia Kifaa Maalum cha Kutazamia Jua.* ***Kukosa kufuata maagizo haya kunaweza kusababisha madhara ya kusikitisha kwako.***

Wataalamu wa masomo ya sayari husema kwamba tukio la kupatwa kwa jua la Agosti 21 2017 litakuwa ni "kupatwa kwa jua kiukamilifu" lakini ili kuona ukamilifu, itabidi uwe katika eneo ndogo la ardhi ambalo linapitia Marekani (linalojulikana kama "njia ya ukamilifu"). Kama hauko kwenye njia hiyo utaweza tu kuona kupatwa kwa sehemu ya jua! kwahiyo ni muhimu sana kujua kama uko kwenye eneo la njia ya ukamilifu na utaelezewa mbinu utakayoitumia.



*Njia ya ukamilifu*

# MWONGOZO MFUPI WA KUTUMIA

# MAELEKEZO YA KINA

Neno "Kifaa Maalum cha Kutazamia Jua", kama kilivyotumiwa katika nakala hii kinaeleweka kuwakilisha "Solar Viewer" kilichozungumziwa kwenye taarifa ya makataa ya lugha ya Kingereza katika ukurasa wa kwanza wa nakala hii.

Matumizi yako ya kutumia Kifaa Maalum cha Kutazamia Jua yanahusisha makubaliano ya kisheria. Ni sharti ufuate barabara na kwa ukamilifu maelezo yote, ushauri, na mwongozo ulio katika nakala ya maelezo ili kutumia Kifaa Maalum cha Kutazamia Jua wakati wowote unapoangalia jua. Ikiwa hauelewi maelezo hayo au hauwezi kuyazingatia barabara na kwa ukamilifu, au haukubaliani na masharti yake, basi unaagizwa na kushauriwa usijaribu kutazama jua wakati wowote ule.

© 2014-2017
Eclipse2017.org, inc.

# *MWONGOZO MFUPI WA KUTUMIA KIFAA MAALUM CHA KUTAZAMIA JUA*

*Mwongozo huu mfupi umedondolewa kutoka kwa mkusanyiko wa maelezo kamili yaliyoandikwa kwa Kiswahili, ambayo sharti uyasome, uelewe na ukubaliane nayo yote ili kutumia Kifaa Maalumu cha Kutazamia jua lililo katika tukio la kupatwa.*

1) **Anagalia eneo lako katika http://tinyurl.com/find-times, ili kubaini kama tukio la kupatwa kwa jua litakuwa kamili huko, na takriban wakati wa mapatano ya tukio lisilo kamili na (kama zinatumika) jumla ya awamu za eneo hilo.**
2) **Tukio kamili la kupatwa kwa jua ni la kuvutia sana lakini unaweza tu kulifurahia kikamilifu kama utakuwa kwenye "njia ya tukio kamili" – ambayo iko katika upana wa kama maili mia moja pekee. Ikiwa haitawezekana kushuhudia tukio kamili kwenye eneo ulilopanga, tunakushauri uweze kufika kwenye eneo lililo katika mapitio/njia ya tukio kamili!**
3) **Kutumia Kifaa Maalum cha Kutazamia Jua, ili kuangalia kupatwa kwa jua, shika lensi ya Kifaa Maalum cha Kutazama jua moja kwa moja mbele ya macho yako ili kuyakinga kutokana na madhara ya kutazama jua moja kwa moja.**
4) **Wakati unapopaswa kutumia Kifaa Maalum cha Kutazama Jua:**
   a. **Kama tukio la kupatwa kwa jua HALITAKUWA kamili katika eneo lako, basi litazame kupitia Kifaa Maalum cha Kutazamia Jua kila wakati. UNAHATARISHA MACHO YAKO KUPATA MADHARA YA KUDUMU KWA KUTAZAMA JUA BILA KINGA YA MACHO INAYOFAA!**
   b. **Kama tukio la kupatwa kwa jua LITAKUWA kamili kwenye eneo lako, basi ni SHARTI utazame jua kupitia Kifaa Maalum cha Kutazamia Jua wakati wowote sehemu ya jua iliyo na mwanga mkuu – hata kama ni kipande kidogo tu – inapoonekana. UNAHATARISHA MACHO YAKO KUPATA MADHARA YA KUDUMU IKIWA UTAKOSA KUFUATA AGIZO HILI!**
      i. **Hata hivyo, kwa kipindi kifupi cha tukio kamili PEKEE, wakati hakuna sehemu yoyote angavu ya jua inayoonekana unatakiwa kutazama tukio kamili la kupatwa kwa jua bila kutumia Kifaa Maalum cha Kutazama Jua.**
      ii. **Ukweli ni kwamba, ukijaribu kutumia Kifaa Maalum cha Kutazamia Jua wakati wa tukio la kupatwa kamili hautaweza kuona chochote!**
      iii. **Ni SHARTI uanze kutumia tena Kifaa Maalum cha Kutazama Jua kama tu tukio kamili linapokamilika na ile sehemu angavu ya jua imeanza kuonekana tena.**
5) **Kwa maneno mengine,**

**KAMA SEHEMU YOYOTE YA DISKI ANGAVU YA JUA INAPOANZA KUONEKANA, NI *SHARTI* UANGALIE JUA KWA KIFAA MAALUM CHA KUTAZAMA JUA!**

*© 2014-2017*
*Eclipse2017.org, inc.*

## *MAAGIZO YA KINA YA KUTUMIA KIFAA MAALUM CHA KUTAZAMIA JUA*

Kwanza, kuna baadhi ya maneno ambayo unapaswa kuyaelewa!

Kwa kila tukio la kupatwa kwa jua na kila eneo duniani, kuna maneno yanayotumiwa kuelezea matukio maalum. Haya yanafahamika kama:

| *Jina la tukio* | *Maelezo ya tukio* | *Inavyodhihirika* (tukio la kupatwa kwa jua lililo kamili) | *Inavyodhihirika* (tukio la kupatwa kwa jua lisilo kamili) |
|---|---|---|---|
| **C1** | **Mwanzo wa awamu isiyo kamili** |  |  |
| **C2** | **Mwanzo wa tukio kamili** |  | ** Halishuhudiwi! ** |
| ***Katikati ya kupatwa*** | **Kipindi cha katikati cha kupatwa** |  |  |
| **C3** | **Mwisho wa tukio kamili** |  | ** Halishuhudiwi! ** |
| **C4** | **Mwisho wa awamu isiyo kamili** |  |  |

© 2014-2017
Eclipse2017.org, inc.

## *1) MAELEZO YA KUTUMIA KIFAA MAALUM CHA KUTAZAMA JUA*



1) [*kama zinatumika*] Fungua Kifaa Maalum cha Kutazamia Jua kwa uangalifu.
2) Tunza Kifaa Maalum cha kutazama Jua wakati hakitumiki.
3) Kagua Kifaa Maalum cha Kutazama Jua kabla ya kukitumia; kama filamu ya lensi imeharibika au kujikunja kwa njia yoyote, basi kata Kifaa Maalum cha Kutazama Jua na kukiharibu, na upate kingine kisichoharibika.
4) Ikiwa filamu ya lensi imeharibika kwa vyovyote vile, usitumie Kifaa Maalum cha Kutazama Jua wakati wowote ule.
5) Usitoe filamu ya lensi kutoka kwenye Kifaa Maalum cha Kutazama Jua na usitumie filamu ya lensi iliyotolewa kwa Kifaa Maalum cha Kutazama Jua kwa vyovyote vile.
6) Lensi ya Kifaa Maalum cha Kutazama Jua iliyoingizwa kama inavyostahili na isiyoharibika inaweza kukinga viwango hatari vya mwangaza unaoonekana,na hata miale hatari ya UV na miale mingine ya jua. Hivyo basi ni salama kabisa kutumia Kifaa Maalum cha Kutazama Jua, kama ilivyoagizwa katika maelezo haya kulitazama jua wakati wowote ule.Hakuna "miale ya kupatwa kwa jua" isiyo ya kawaida ambayo inaweza kuongeza au kupunguza madhara ya kutazama jua wakati wake wa kupatwa.
7) **Ni sharti utumie Kifaa Maalum cha Kutazama Jua jinsi ilivyoelezwa hapa, ili kulitazama jua kwa usalama, wakati sehemu YOYOTE angavu ya diski ya jua inaonekana. Hii ni kweli licha ya nyakati zozote za matukio ya kupatwa kwa jua (yanayojulikana kama, "C2" na "C3" jinsi ilivyoelezewa hapo juu) ambayo umeshuhudia mahali popote.**
8) Usitumie Kifaa Maalum cha Kutazamia Jua pamoja na darubini, kikuzi, kamera, lensi, kioo, au ("chombo cha kutumiwa machoni"), kifaa au kitu chochote ambacho kinaweza kupitisha au kuelekeza mwangaza.
9) Usielekeze chombo kama hicho kinachotumiwa machoni kwa jua na usije ukatazama umbo la Jua moja kwa moja ukitumia chombo chochote cha macho kinachoelekezwa kwa jua ama kwa njia yoyote ile kinachoweza kuvuta, kuelekeza au kurudisha mwanga wa jua.
10) Usikubali Kifaa Maalum cha Kutazama Jua kitumiwe na wanyama au mtu yeyote asiyeweza kuona vyema, asiyeweza kusoma, kuelewa na kukubaliana na maagizo ya matumizi salama ya Kifaa Maalum cha Kutazama Jua au kukubali kuwajibika kisheria kwa matokeo yanayoambatana na majukumu yake.



11) Kutumia Kifaa Maalum cha Kutazama Jua:

    Weka Kifaa Maalum cha Kutazama Jua kati ya macho yako na jua kisha utazame kupitia lensi ya Kifaa cha Kutazama Jua isiyoharibika, ukielekea jua, huku ukiweka kabisa lensi ya Kifaa Maalumu cha Kutazama Jua kati ya macho yako na jua kila wakati. Kwa kifaa cha Kutazama jua kilicho na umbo la miwani ya kijikaratasi kigumu, unaweza kukikuja kijikaratasi ili kuvalia Kifaa Maalum cha Kutazama Jua jinsi unavyovalia miwani ya kawaida. Usije ukatazama jua mojakwa moja ikiwa bado hailko katika tukio la kupatwa kamili. (yaani, wakati kati ya C2 na C3 kama vile utakavyoona kwenye chati iliyoko hapa chini, kama majira hayo yanawezekana kwenye eneo lako), isipokuwa kutazama moja kwa moja kupitia kwa lensi ya Kifaa Maalum cha Kutazama Jua kisichoharibika.
12) Usitumie kifaa au chombo kingine kujikinga unapotazama jua, ila tu lensi za Kifaa Maalumu cha Kutazama Jua ambazo zimewekwa kwenye fremu zake toka kiwandani.
13) Ikiwa una swali lolote kuhusu maelezo haya, tafadhali wasiliana na Eclipse2017.org kwenye http://tinyurl.com/viewer-questions.

© 2014-2017
Eclipse2017.org, inc.

## 2) JIFAHAMISHE NA NYAKATI ZA MUTUKIO YA KUPATWA KWENYE JUA YA ENEO LAKO

Kulingana na habari iliyotolewa kwenye http://tinyurl.com/find-times kwa eneo lako, kamilisha taarifa ifuatayo:

***Katika eneo langu, kupatwa kwa jua ni:***

| | |
|---|---|
| **NI KAMILI** | **SI KAMILI** |

*(Weka mviringo kwa moja)*

| | |
|---|---|
| **Kama kupatwa kwa jua *NI KAMILI* katika eneo lako, basi fuata maelezo yaliyomo kwenye**<br><br>**“Kupatwa kwa jua *NI KAMILI* katika eneo langu”**<br><br>**sehemu hapa chini:** | **Kama kupatwa kwa jua *SI KAMILI* katika eneo lako, basi fuata maelezo yaliyomo kwenye**<br><br>**“Kupatwa kwa jua *SI KAMILI* katika eneo langu”**<br><br>**sehemu hapa chini:** |

© 2014-2017
Eclipse2017.org, inc.

## ** KUPATWA KWA JUA *NI KAMILI* KATIKA ENEO LANGU **

Uko katika njia ya tukio kamili, na utashuhudia tukio adimu na la kuvutia! Ni muhimu sana uweze kujua ni lini tukio la kupatwa kwa jua ni kamili kwenye eneo lako. Utaweza kufanya hivyo kwa kuangalia nyakati kama vile umeona hapa chini na pia kwa sababu hakutakuwa na sehemu angavu inayoonekana kwenye diski ya jua wakati wa tukio kamili.

1) Kulingana na habari iliyotolewa na http://tinyurl.com/find-times kuhusiana na eneo lako haswa, andika nyakati unazotazamia kutukia kwa kila tukio la kupatwa kwa jua kama ilivyoandikwa hapa chini (tafadhari hakikisha unaweka sawa muda wa ukanda wako!):

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| ***Kabla ya C1*** | * Hakuna kupatwa kwa jua * | |  |  | **SHARTI** utumie Kifaa Maalum cha Kutazamia Jua |
| ***C1*** | **Awamu isiyo kamili kuanza:** | |  |  | **SHARTI** utumie Kifaa Maalum cha Kutazamia Jua |
| ***C2*** | **Awamu kamili kuanza:** | |  |  | **Baada ya C2**, unaweza kutazamia kwa macho wazi |
| ***Katikati ya kupatwa*** | **kutukia** | |  |  | **Unaweza kutazama kwa macho yaliyo wazi!** |
| ***C3*** | **Awamu kamili kumalizika:** | |  |  | **SHARTI** utumie Kifaa Maalum cha Kutazamia Jua tena |
| ***C4*** | **Awamu isiyo kamili kumalizika:** | |  |  | **SHARTI** utumie Kifaa Maalum cha Kutazamia Jua |
| ***Baada ya C4*** | * Hakuna kupatwa kwa jua * | |  |  | **SHARTI** utumie Kifaa Maalum cha Kutazamia Jua |

2) Ingawa uko katika eneo la tukio kamili, bado itakulazimu kutumia Kifaa Maalum cha Kutazama Jua unapoangalia jua kila wakati kabla ya C2 au baada ya C3, wakati tukio la kupatwa kwa jua siyo kamili.

*© 2014-2017*
*Eclipse2017.org, inc.*

3) Unaweza kutazama jua moja kwa moja kwa macho yaliyo wazi (bila kutumia Kifaa Maalum cha Kutazama Jua) IKIWA TU:
    a. Ikiwa tukio la kupatwa kwa jua ni kamili katika eneo lako (uko kwenye “njia/pitio”), NA
    b. Wakati wa tukio kamili (takriban muda kuanzia C2 hadi C3 kwenye eneo lako kama ulivyoona hapo juu), NA
    c. uweze kuwa **Wakati wowote sehemu ya diski angavu ya jua imefunikwa na mwezi kabisa.**

Nyakati halisi za ukamifu zitatofautiana pakubwa kulingana na eneo lako haswa na itabidi uwe umebainisha na kuweka kumbukumbu ya muda unaokisia kabla ya matukio. Nyakati unazoweka kwa kumbukumbu hapa juu ni zile zinazokaribia!

4) Tena, licha ya nyakati zilizotajwa katika nakala iliyoko hapa juu au zilizotolewa kutoka sehemu zingine zozote, **sharti utazame jua ukitumia Kifaa Maalum cha Kutazama Jua wakati WAKATI WOWOTE SEHEMU ya diski angavu ya jua iliyo inapoonekana**.

5) Maelezo haya yanafuatwa na michoro ya ziada yenye uwazi ili kukusaidia kuelewa.

---

***Ni Sharti usome, uelewe na uzingatie taarifa zifuatazo:***

## INANILAZIMU NIFUATE MAELEZO YOTE KUHUSU MATUMIZI YA KIFAA MAALUM CHA KUTAZAMIA JUA ILI NIWEZE KUKITUMIA KWA NJIA ILIYO SALAMA.

# IKIWA KUNA SEHEMU YOYOTE YA DISKI ANGAVU YA JUA INAONEKANA, SHARTI NITUMIE KIFAA MAALUM CHA KUTAZAMA JUA NINAPOTAKA KUANGALIA JUA.

© 2014-2017
Eclipse2017.org, inc.

## ** TUKIO LA KUPATWA KWA JUA *SI KAMILI* KWENYE ENEO LANGU **

Hauko kwenye njia ya tukio Kamili, na basi hautashuhudia kivutio cha tukio kamili la kupatwa kwa jua. (Tunakushauri kwenye njia ya tukio kamili ili uweze kushiriki katika kivutio hiki cha kushangaza!)

1) Kulingana na habari iliyotolewa kwenye http://tinyurl.com/find-times kuhusu eneo lako andika nyakati unazokisia kila tukio la kupatwa kwa jua kama ilivyonakiliwa hapa chini (tafadhari hakikisha unaweka sawa muda wa ukanda wako!):

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| ***Kabla ya C1*** | * Hakuna kupatwa kwa jua * | |  |  | **SHARTI** utumie Kifaa Maalum cha Kutazamia Jua |
| ***C1*** | **Awamu isiyo kamili kuanza:** | |  |  | **SHARTI** utumie Kifaa Maalum cha Kutazamia Jua |
| ***Katikati ya kupatwa*** | **kutukia:** | |  |  | **SHARTI** utumie Kifaa Maalum cha Kutazamia Jua |
| ***C4*** | **Awamu isiyo kamili kumalizika:** | |  |  | **SHARTI** utumie Kifaa Maalum cha Kutazamia Jua |
| ***Baada ya C4*** | * Hakuna kupatwa kwa jua * | |  |  | **SHARTI** utumie Kifaa Maalum cha Kutazamia Jua |

*(Zingatia kwamba awamu za C2 na C3 hazijaratibiwa kwa kuwa tukio la kupatwa kwa jua si kamili kwenye eneo lako!)*

2) **Kwa kuwa tukio la kupatwa kwa jua sio kamili mahali ulipo, ni sharti utumie Kifaa Maalum cha Kutazamia Jua KILA WAKATI unapoangalia jua.** Tena tunakushauri uweze kusafiri hadi kwenye njia ya tukio kamili. Kumbuka kubeba Kifaa Maalum cha Kutazamia Jua ili uweze kushuhudia awamu zisizo kamili za kupatwa kwa jua.

3) Maelezo haya yanafuatwa na michoro ya ziada yenye uwazi ili kukusaidia kuelewa.

---

***Ni Sharti usome, uelewe na uzingatie taarifa zifuatazo:***

**INANILAZIMU NIFUATE MAELEZO YOTE KUHUSU MATUMIZI YA KIFAA MAALUM CHA KUTAZAMIA JUA ILI NIWEZE KUKITUMIA KWA NJIA ILIYO SALAMA.**

**NI SHARTI NITUMIE KIFAA MAALUM CHA KUTAZAMA JUA KILA WAKATI NINAPOANGALIA JUA.**

*© 2014-2017*
*Eclipse2017.org, inc.*